# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara yaChukwani, Buyu,
70490 MjiniMagharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, aliyetupa neema ya uhai na uzima, na kutupa fursa ya kukutana ndani ya Baraza hili katika muendelezo wa majukumu yetu ya kitaifa.

Shukurani za pekee nazitoa kwako Pamoja na wasaidizi wako kwa namna mnavyoliendesha Baraza hili kwa hekima, busara na weledi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa dhati kabisa, tunampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kutuletea dhana ya Uchumi wa Buluu na kuunda Wizara ya kuisimamia dhana hiyo kikamilifu kwa ajili ya kupanga na kusimamia ulinzi, uendelezaji na uvuvnaji wa rasilimali na mazao ya baharini kwa maslahi mapana ya vizazi vya sasa na vijavyo. Ni ukweli usiopingika kuwa, usimamizi bora wa sekta zilizomo kwenye Wizara hii ni chachu ya maendeleo kwa nchi yetu na ni wajibu wa kila mmoja wetu kuunga mkono utekelezaji wa dhana hiyo kwa nafasi yake.

**Mheshimiwa Spika,**

Pongezi mahsusi tunazitoa kwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Mheshimiwa Shaaban Ali Othman kwa uongozi wake imara ambao umepelekea watendaji wote wa Wizara hii kuanzia Katibu Mkuu Kepteni Hamad Bakari Hamad, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Zahor Kassim Mohammed pamoja na watendaji wengine wote kuwa na mashirikiano mazuri yaliyoiwezesha Kamati yetu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, tunawashukuru watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Bajeti inayoongozwa na mwanamama Jasiri Kamishna Zena Mahmoud Hassan. Chini ya muongozo na usimamizi wa Idara hii, Kamati iliweza kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ni imani yetu kuwa, mashirikiano baina yetu yatazidi kuimarika siku hadi siku na kuleta wepesi wa kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Natoa shukurani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati yangu ambao wamejitolea kwa nguvu zao zote kuhakikisha shughuli hii muhimu ya upitiaji wa Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inafanyika kwa ufanisi na kukamilika kwa wakati uliopangwa. Kwa heshima naomba Kuwatambulisha mbele ya Baraza lako kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti

3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Mohammed Ali Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe

Aidha, Kamati inafanya kazi kwa kushirikiana na makatibu watatu na msaidizi mmoja ambao ni:

1. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu
2. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
3. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
4. Ndg. Azmina Khamis Hamad - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imetekeleza jukumu lake la kujadili na kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya fungu L02 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 tarehe 29/4/2025 ikiwa ni utakelezaji wa matakwa ya Kanuni ya 101 ya Kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2024, na kupendekeza marekebisho madogo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu maoni ya Kamati kuhusu mafungu ya bajeti ya fungu L02 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Fungu Kuu moja la L02 na limepangiwa kutekeleza Programu kuu tatu (3) zenye Programu ndogo saba (7) ambazo kwa ujumla wake zinajumuisha shughuli na huduma zote zinazokusudiwa kutekelezwa na Wizara hii, katika mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajiwa kukusanya jumla ya Tsh. Bilioni 11,273,214,000 kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Aidha, Wizara inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 172,033,961,000 Kati ya fedha hizo Tsh. Bilioni 14,952,100,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na Tsh. Bilioni 157,081,861,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Ongezeko la makadirio ya mapato yatakayokusanywa na Wizara hii kutoka Tsh. Bilioni 5,921,734,000 mwaka wa fedha 2024/2025 hadi Tsh. Bilioni 11,273,214,000 kwa mwaka 2025/2026 ni jambo lililoitia shaka Kamati yetu na kupatiwa ufafanuzi kwamba Wizara imechukuwa hatua mbali mbali ili kuimarisha makusanyo hayo ikiwa ni Pamoja na kuibua vyanzo vipya vya mapato, kurekebisha tozo kwenye viingilio vya maeneo ya hifadhi ya Bahari Pamoja na kuimarisha mifumo ya makusanyo na kuwa ni kwa njia ya kielektroniki. Tunaipongeza Wizara kwa kuwa wabunifu na tunaiomba iweke mikakati imara itakayopelekea kutimiza malengo yaliyowekwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwakuwa suala la uhifadhi wa Bahari ni muhimu kwa matumizi endelevu ya rasilimali zilizomo kwa vizazi vya sasa na vijavyo, na kwakuwa Serikali imetenga jumla ya Tsh. Bilioni 3,700,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa juhudi za makusudi za kuhifadhi maeneo yetu ya Bahari, Kamati inaiomba Serikali kuwaangalia wavuvi wetu kwa jicho la huruma kwa kuwapatia nyenzo nyengine za kujitafutia maisha ikiwemo kuanzishiwa vizimba vya ufugaji ili kuendeleza familia zao.

Aidha, Kamati inaipongeza Wizara kwa kufanikiwa kukamilisha utayarishaji wa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wavuvi, vyombo vya uvuvi Pamoja na ukataji wa leseni za uvuvi ambao tayari umeanza kufanya kazi. Mfumo huo utaonesha idadi kamili ya wavuvi waliopo nchini na kuweza kuwapangia mipango ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaunga mkono mkakati wa Wizara kwa kuendeleza sekta ya uvuvi kupitia ujenzi wa viwanda vya uongezaji wa thamani ya mazao ya baharini ambao unakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 51,000,000,000 na utatekelezwa katika huduma (HL 02020113). Kupitia viwanda hivyo, bidhaa zitakazozalishwa zitakuwa ni zenye thamani zaidi na zenye kuhitajika sokoni na kutumika ndani na nje ya nchi. Kamati inaiomba Wizara kusimamia vyema ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mazao ya baharini kilichopo Kama kwa Unguja na Ndagoni kisiwani Pemba na kuhakikisha vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya utendaji wa viwanda hivyo vinapatikana kwa wakati ili kufikia malengo yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu iliarifiwa kuwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Taasisi ya Utafiti wa uvuvi na Maliasili za baharini Zanzibar (ZAFIRI) inasimamia uanzishwaji wa Maabara ya Uboreshaji wa Mbegu za Mwani (Seaweed Tissue Culture Laboratory) ili kuzalisha mbegu zitakazohimili mabadiliko ya tabia nchi na mambo mengine ya kimazingira yanayoathiri zao la mwani nchini mwetu. Tunaipongeza Wizara kwa hatua hiyo muhimu ambayo itpelekea tafiti mbalimbali kufanyika na kuibua mbegu bora za mwani ambazo zitatoa tija nzuri wa wakulima. Ni Imani yetu kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi itaharakisha mchakato wa kuwapata wataalamu wa kuiendesha maabara hii na itaandaa utaratibu mzuri wa ugawaji wa mbegu hizo Pamoja na usimamizi wa wakulima mashambani mwao ili kuwakomboa wakulima ambao wengi wao ni akina mama.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 makadirio ya mapato yatakayokusanywa na Wizara kwa upande wa Pemba yanatarajiwa kupungua kutoka Tsh. Milioni 592,173,000 hadi Tsh. Milioni 428,664,000. Kamati ilihoji juu ya mapungufu hayo na kuelezwa kuwa, yanatokana na uwekaji wa kumbukumbu za mazao yanayosafirishwa nje ya nchi kuwekwa kwa pamoja makao makuu ya Wizara yaliyopo Unguja. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri kumbukumbu za mapato ya uhaulishaji wa mazao na rasilimali za baharini mapato yake yaonekane katika eneo la uzalishaji wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na

kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili na kutoa mapendekezo hayo na hatimae kuipitisha Bajeti hii ili kumruhusu Mheshimiwa Waziri kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**MheshimiwaS pika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu naiunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

…..……………..…….…….

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu,
Makamo Mwenyekiti,
Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**